

Alisema ili kukuza biashara muhimu wazalishaji wakathibitisha ubora wa bidhaa zao TBS,

kwenye... kama zinakidhi ubora," alisema Mwakalinga na kuongeza:

Kuhusu hatua zinazochukuli- kiuchumi.

Bil 1.4/- kujenga soko la samaki Kasanga

Na Muhidin Amri, Kalambo

SERIKALI imetoa Sh bilioni 1.4 kwa ajili ya kujenga soko la kisasa la kuuzia samaki katika Bandari ya Kasanga, Halmashauri ya Wilaya Kalambo mkoani Rukwa.

Soko hilo litasaidia kuongeza hamani ya samaki na kudhibiti potevu wa mapato unaofanywa na wafanyabiashara wanaosafirisha samaki kwa njia ya panya kwenda nchi zote ikiwemo Zambia na Jamhuri ya Demokrasia ya Congo(DRC). Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Kalambo, Shafi

Mpenda alisema ujenzi wa soko hilo umefikia asilimia 95 na kwamba ujenzi wa soko la kisasa la samaki la Kasanga umekuja baada ya soko la awali kuzingirwa na maji mwaka 2021 kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Aidha alisema halmashauri ya wilaya kupitia mapato yake ya ndani imenunua boti mbili za kisasa kwa ajili ya shughuli za doria kwenye Ziwa Tanganyika ili kukomesha vitendo vya uvuvi haramu na kusaidia pale yanapotokea maafa kwenye ziwa.

Mpenda amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa moyo wa upendo kwa kuwakumbuka

wavuvi wanaofanya shughuli zao katika Ziwa Tanganyika na kutoa fedha ambazo zinaenda kumaliza kilio cha muda mrefu cha wavuvi na wafanyabiashara kukosa soko la kuuzia samaki.

Kwa upande wake Mkuu wa Idara ya Uchumi, Mipango na Uratibu wa Halmashauri ya Wilaya Kalambo, Erasto Mwasanga alisema Soko la Samaki Kasanga litawasaidia wavuvi kuwa na mahali pazuri na uhakika kwa ajili ya kufanya shughuli zao.

Alisema soko hilo litakomesha vitendo vya kusafirisha samaki kwa njia ya panya ambavyo vinasababisha serikali kushindwa kukusanya ushuru unaostahili na hivyo kuioko-

sesha mapato yake.

Aliongeza kuwa litakuwa na vizimba vyenye uwezo wa kuhudumia wafanyabiashara 100 kwa wakati mmoja, jokoftu la kuhifadhi samaki wabichi kabla ya kupelekwa kwenye masoko yaliyopo ndani na nje ya Mkoa wa Rukwa.

Kwa mujibu wa Mwasanga, awali haikuwa rahisi kwa wavuvi na wafanyabiashara kusafirisha mazao ya samaki kwenda kwenye miji mikubwa kutokana na kukosekana kwa soko lenye miundombinu ya kisasa.

Alisema soko hilo litakopokamilika wafanyabiashara watasafirisha samaki wabichi kwenda maeneo mengine kwa urahisi na amewataka

wavuvi na jamii kutunza na kulinda miundombinu na kutumia fursa ya uwepo wa soko hilo kuongeza mazao ya samaki, kwani serikali imetumia fedha nyingi katika kutekeleza mradi huo.

Mvuvi Martin Honde alisema uwepo wa soko hilo utasaidia wavuvi kuwa na soko la uhakika badala ya kuhangaika huku na kule na kupata hasara kutokana na gharama za usafirishaji.

Mvuvi mwingine Adam Raymond ameionba serikali kumbana mkandarasi anayetekeleza mradi huo ili soko likamilike haraka na waweze kuitumia kuuza samaki na bidhaa nyingine za uvuvi.